**HOTUBA YA MHE. HAMZA SAIDI JOHARI, MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI KATIKA UZINDUZI WA KAMATI YA USHAURI WA KISHERIA NGAZI YA MKOA NA WILAYA NA KLINIKI YA SHERIA KWA MKOA WA SINGIDA TAREHE 19 MEI, 2025 KATIKA UWANJA WA STENDI YA ZAMANI MJINI SINGIDA**

---

- ✓ ***Mhe. Halima O. Dendego, Mkuu wa Mkoa wa Singida;***
- ✓ ***Mhe. Dkt. Damas Daniel Ndumbaro (Mb.), Waziri wa Katiba na Sheria;***
- ✓ ***Katibu Tawala Mkoa wa Singida,***
- ✓ ***Kamati ya Usalama ya Mkoa,***
- ✓ ***Wahe. Wakuu wa Wilaya,***
- ✓ ***Wahe. Wenyeviti wa Halmashauri mliopo***
- ✓ ***Makatibu Tawala wa Wilaya,***
- ✓ ***Wakurugenzi wa Halmashauri,***
- ✓ ***Wakuu wa Mashirika ya Umma, Taasisi na Idara za Serikali mliopo;***
- ✓ ***Ndugu Bavoo Junus, Rais wa Chama cha Mawakili wa Serikali Tanzania;***
- ✓ ***Bi. Mercy Ngowi Wakili wa Serikali Mkoa wa Singida na Mwenyekiti wa Kamati ya Ushauri Mkoa,***
- ✓ ***Wajumbe wa Kamati ya Ushauri wa Kisheria ya Mkoa na Wajumbe wa Kamati za Ushauri za Wilaya mliopo,***
- ✓ ***Bi. Lela Salum Mwakilishi wa Chama cha Mawakili wa Serikali Mkoa wa Singida;***
- ✓ ***Viongozi na Wawakilishi wa Chama cha Wanasheria wa Tanganyika (Tanganyika Law Society) na vyama vingine vya kitaaluma;***

- ✓ ***Wakuu na wawakilishi wa Vyuo vikuu, Vyuo vya Mafunzo na shule;***
- ✓ ***Wakurugenzi, Wakurugenzi Wasaidizi, Wakuu wa Idara za Sheria, Mkuu wa Mashtaka wa Mkoa na Wilaya, Wakili wa Mkoa kutoka Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Mkoa;***
- ✓ ***Maafisa Sheria na Mawakili wa Serikali wa ngazi mbalimbali mliopo;***
- ✓ ***Viongozi wote wa Vyama vya Siasa mliopo;***
- ✓ ***Viongozi wote wa dini mliopo;***
- ✓ ***Wananchi wa mkoa wa Singida;***
- ✓ ***Ndugu Wanahabari na wageni wote waalikwa mliopo;***
- ✓ ***Mabibi na Mabwana;***

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA..........**

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kukutana hapa siku ya leo katika uzinduzi wa Kamati ya Ushauri wa Kisheria ngazi ya Mkoa na Wilaya pamoja na Kliniki ya Sheria kwa Mkoa wa Singida. Kama ambavyo viongozi wetu wa dini walivyotuombea, tunamwomba Mwenyezi Mungu atuongoze ili tuweze kuanza na kumaliza uzinduzi huu na kliniki ya sheria kwa salama, amani na mafanikio.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Kwa dhati ya moyo wangu, naomba nikushukuru sana wewe binafsi kwa kukubali kutenga muda wako adhimu na kukubali kuwa Mgeni Rasmi katika

tukio hili muhimu la Uzinduzi wa Kamati ya Ushauri wa Kisheria ngazi ya Mkoa na Wilaya katika Mkoa wa Singida ambapo uzinduzi huu utafuatiwa na Kliniki ya Sheria itakayoendeshwa kuanzia leo tarehe 19 hadi tarehe 25 Mei, 2025 ambapo wananchi watapata fursa ya kupata huduma za kisheria bila malipo.

Naomba kuishukuru Ofisi yako na viongozi mbalimbali wa mkoa huu pamoja na wanachi wa mkoa wa Singida kwa mapokezi mazuri mliyotupatia tangu tulipofika hapa mkoani Singida. Tumefurahi sana kwa upendo wa dhati mliotuonesha. Kwa namna ya pekee pia nawashukuru sana wageni wetu na wananchi wote kwa kutenga muda wenu na kujitokeza na kuungana nasi katika uzinduzi huu. **Ahsanteni sana.**

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Napenda kuishukuru sana Sekretarieti ya mkoa wa Singida chini ya Katibu Tawala wa mkoa, Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali Bw. Samwel Maneno, Menejimenti ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Chama cha Mawakili wa Serikali na Kamati ya Maandalizi kwa kufanikisha maandalizi ya uzinduzi huu na kliniki ya Sheria. Nathamini sana muda wao walioutoa katika kuhakikisha shughuli hii inafanikiwa.

Aidha, napenda kuwashukuru sana Mawakili wote wa Serikali na Mawakili wa Kujitegemea waliopo hapa kwa kutenga muda wao na kusafiri kutoka maeneo mbalimbali kuja kushiriki katika uzinduzi huu na kujitolea kutoa ushauri wa kisheria na elimu ya sheria kwa wananchi watakaojitokeza kuwasilisha changamoto zao za kisheria katika kipindi chote cha Kliniki ya sheria.

Niwashukuru sana waajiri wa Mawakili hao kwa kuwaruhusu kutoka katika vituo vya kazi na kuwawezesha kushiriki pamoja nasi katika shughuli hii.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Mwanasheria Mkuu wa Serikali ndiye Mshauri Mkuu wa Serikali katika masuala yote ya sheria. Hii ni kwa mujibu wa Ibara ya 59(3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Kifungu cha 8 cha Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Sura ya 268.

Aidha, majukumu ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali hayaishii katika kuishauri Serikali bali yanaendelea hadi kutoa ushauri kwa wananchi pia. Ibara ya 8 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeeleza kuwa, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni nchi inayofuata misingi ya demokrasia na haki ya kijamii, kwa hiyo wananchi ndio msingi wa mamlaka yote na Serikali itapata Madaraka na mamlaka yake yote kutoka kwa wananchi. Pia, Ibara hiyo imeendelea kueleza kuwa Serikali itawajibika kwa wananchi. Hivyo basi, ni wazi kuwa ninawajibika kwa wananchi kama ilivyoelezwa katika Ibara ya 8.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Niseme tu kwamba, moja ya njia inayotumiwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuwajibika kwa wananchi ni kutoa ushauri na msaada wa kisheria kwa wananchi kwa kutumia Kamati za Ushauri wa Kisheria kwa ngazi ya Mkoa na ngazi za Wilaya. Hivyo, Ofisi yangu ilitoa Mwongozo wa Uanzishwaji wa Kamati za Ushauri wa Kisheria za Mikoa na Wilaya kwa mujibu wa Kifungu

cha 21 cha Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Lengo kuu la uanzishwaji wa Kamani za Ushauri wa Kisheria kwa ngazi ya Mkoa na Wilaya ni kurahisisha usimamizi wa utoaji wa ushauri wa kisheria kwa wananchi katika maeneo husika.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Kwa ngazi ya Mkoa, Kamati za Ushauri wa Kisheria inaundwa na wajumbe wafuatao:

1. Mwenyekiti ambaye ni Wakili wa Serikali wa Mkoa kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali au Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na ikiwa Ofisi hizi hazijafunguliwa katika Mkoa husika basi atatoka Ofisi ya Taifa ya Mashtaka;

2. Katibu ambaye ni Mkuu wa Kitengo cha Sheria kutoa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa;

3. Mjumbe mmoja kutoka Ofisi ya Taifa ya Mashtaka;

4. Mjumbe mmoja kutoka Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali;
5. Wajumbe wawili kutoka katika vyombo vya ulinzi na usalama ambao ni wanasheria. Wajumbe hawa huteuliwa na Mkuu wa Mkoa; na

6. Wakili wa Serikali kutoka katika taasisi nyingine ya Serikali katika Mkoa husika.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Kwa ngazi za Wilaya, Kamati hii inawajumbe wafuatao:

1. Mwenyekiti ambaye ni Mwakilishi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali au Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali au Ofisi ya Taifa ya Mashtaka na ikiwa ofisi hizo hazijafunguliwa katika Wilaya husika, atakuwa Mkuu wa Kitengo cha Sheria kutoka katika Halmashauri ya Jiji, Manispaa, Mji au Wilaya husika;

2. Wakili wa Serikali kutoka TAKUKURU au Wakili wa Serikali kutoka katika taasisi ya Serikali iliyo katika Wilaya husika;

3. Wakili wa Serikali kutoka Ofisi ya Taifa ya Mashtaka;

4. Wakili wa Serikali kutoka Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali;

5. Wajumbe wawili kutoka katika vyombo vya ulinzi na usalama ambao ni wanasheria. Wajumbe hawa huteuliwa na Mkuu wa Wilaya; na

6. Wakili wa Serikali kutoka katika taasisi nyingine ya Serikali katika Wilaya husika.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Wenyeviti wa Kamati hizi katika ngazi ya Mkoa na Wilaya watakuwa na mamlaka ya kuongeza wajumbe wawili ambao siyo Mawakili wa Serikali pale itakapohitajika kulingana na uhalisia wa jambo linaloshughulikiwa na Kamati. Mwongozo unaelekeza yote haya yatafanyika kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa na Ofisi za Wakuu wa Wilaya.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Kama nilivyoeleza hapo awali, Uzinduzi wa Kamati hii utafuatiwa na Kliniki ya sheria kuanzia leo hadi tarehe 25 Mei, 2025 ambapo huduma za ushauri wa kisheria zitatolewa kwa wananchi bila malipo. Kliniki hizi za kisheria zinazoratibiwa na kusimamiwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ni utekelezaji wa matakwa ya Ibara ya 8 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo inaelekeza jukumu la Serikali la kuwajibika kwa wananchi. Pia, ni utekelezaji wa maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye amekuwa akituelekeza viongozi wa Serikali mara kwa mara katika kushughulikia na kuzipatia ufumbuzi kero za wananchi tena kwa kuwafikia katika maeneo husika na kuwahudumia. Hivyo basi, Kliniki za sheria zimelenga:

- Kusogeza huduma za sheria karibu na wananchi ambako kutasaidia kuongeza utengamano na utulivu katika jamii na kuchochea maendeleo kwa jamii na taifa kwa ujumla;

- Kuwaongoza wananchi katika taratibu za kupata haki zao pale zinapovunjwa au zinapoonekana kuelekea kuvunjwa na kudumisha utawala bora kwa kuimarisha utawala wa sheria nchini;

- Kutoa elimu ya sheria kwa wananchi na kuongeza ushirikiano miongoni mwa Mawakili wa Serikali na Mawakili wa Kujitegemea katika kushughulikia changamoto mbalimbali za kisheria katika maeneo yao; na

- Kuepusha au kupunguza mashauri yasiyo ya lazima;

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Kwa ujumla Kliniki za Kisheria zimelenga kuipa uhai Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050, inayolenga kuwa na taifa jumuishi lenye ustawi, haki na linalojitegemea. Matarajio ni kuwa na jamii yenye maelewano ambapo wananchi wanafurahia kuwepo kwa amani na haki, na hili litawezekana kupitia kwa programu kama Kliniki za Sheria ambapo wananchi wanapata fursa za kusikilizwa na kutatuliwa changamoto zao na Serikali mapema.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Mpaka sasa Kamati hizo zimekwishazinduliwa katika mikoa mitatu ambayo ni Dodoma, Kilimanjaro na Mwanza na maandalizi kwa ajili ya uzinduzi katika mikoa mingine yanaendelea. Katika mikoa ambayo Kamati hizi zimeshaanza kufanya kazi, zimekuwa msaada mkubwa kwa wananchi na Serikali na tunatarajia kupitia Kamati hizi tutawafikia wananchi katika maeneo yao hasa ya vijijini ambako huduma za kisheria zimekuwa zikipatikana kwa gharama kubwa na wakati mwingine imekuwa vigumu kupata huduma za kisheria katika baadhi ya maeneo.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi;**

Kabla sijahitimisha hotuba yangu, naomba nitoe wito kama ifuatavyo;

i) Mawakili wa Serikali ambao kwa nafasi zao ni viongozi au wajumbe wa Kamati hizi, kujitoa kwa moyo katika kusikiliza malalamiko na kuyatafutia suluhu kwa weledi na umahiri mkubwa;

ii) Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Menejimenti ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuona uwezekano wa kuziwezesha Kamati hizi kutekeleza majukumu yake;

iii) Kamati za Ushauri wa Kisheria za Mikoa na Wilaya, zifuatilie na kutatua changamoto zote zinazoibuliwa wakati wa Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia;

iv) Wananchi kuzitumia Kamati hizi ambazo zitakuwa karibu nao katika Mikoa na Wilaya zao. Kamati hizi zimepewa jukumu la kupokea na kutafuta suluhisho la changamoto mbalimbali za kisheria zinazowakabili Wananchi;

v) Kwa Mikoa na Wilaya ambazo bado hazijakamilisha uundwaji wa Kamati hizo, wajitahidi kukamilisha zoezi hilo mapema. Ofisi yangu itatoa ushirikiano wa kutosha katika kufanikisha kukamilika kwa zoezi hilo ili huduma hizi za ushauri wa kisheria kwa wananchi bila malipo ziweze kuwafikiwa wananchi wa mikoa na wilaya hizo pia.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Mwisho, japo sio kwa umuhimu ninaiomba Ofisi yako na Ofisi za Wakuu wa Wilaya kuendelea kutoa ushirikiano kwa Kamati hizi ili ziweze kutekeleza majukumu yake na kuisadia Ofisi yako na Ofisi za Wilaya katika kuendeleza utawala wa sheria nchini ili kudumisha amani na utengemano katika jamii yetu, jambo litakalowezesha wananchi kuwa na muda wa kutosha wa kufanya

kazi zao za uzalishaji mali bila bughudha yoyote na hivyo kujiongezea kipato na kuinua Uchumi wa mtu mmoja mmoja  na Taifa kwa ujumla.

Sasa naomba nikukaribishe rasmi ili uweze kutoa hotuba yako na kuzindua Kamati ya Ushauri wa Kisheria ya Mkoa wa Singida na Kamati za Ushauri wa Kisheria kwa Wilaya za Singida, Manyoni, Ikungi, Mkalama na Iramba. **Karibu sana!**